*OFISI YA RAIS*
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Shule ya Sekondari Ilboru,
S.L.P. 3014,
ARUSHA.

........................

***SIMU: 0754 090978***
***0719 331255***

Ndg. ..................................

..........................................

..........................................

Ndugu Mwanafunzi,

**YAH: <u>KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO</u>**
**<u>SHULE YA SEKONDARI ILBORU - 2016</u>**

Wanajumuiya wote wa Shule ya Sekondari Ilboru wanakupongeza kwa kuchaguliwa kwako kujiunga na shule hii MAALUM. Ni shule Maalum kwa maana ya mahali pa kusoma vijana wenye vipaji vya hali ya juu kiakili na kitabia. Kwa hiyo basi, unatakiwa usome kwa bidii sana na kuwa na nidhamu wakati wote utakapokuwa shuleni Ilboru, la sivyo itakubidi uondolewe hapa na kutoa nafasi kwa mwanafunzi mwingine mwenye uwezo zaidi. Ni muhimu vile vile uelewe kuwa Serikali yetu imekupatia nafasi katika shule hii maalum kwa lengo la kukuandaa kuja kulitumikia Taifa kama Mtaalam Bingwa na mzalendo.

Shule iko Kaskazini mwa mji wa Arusha, kutoka mjini Arusha, shule hii ipo umbali wa km.2. Gharama za taxi ni kati ya Sh. 6000/= au zaidi. Inategemea wakati utakapowasili mjini Arusha. Kumbuka shule haitawajibika kukulipia gharama hii.

Baada ya pongezi hizo napenda kukujulisha mahitaji ya shule hii.

**1. Vifaa vinavyohitajika shuleni:**

(i) Result slip (Kivuli)
(ii) File/Jalada la kutunzia mitihani
(iii) Mashati mawili meupe (tetron) ya mikono mirefu
(iv) Viatu vya ngozi vyeusi jozi moja – vyenye **gidamu** (kufunga kamba). Visiwe na kisigino kirefu.
(v) Vitabu vya kukazia maarifa – Orodha imeambatanishwa
(vi) Madaftari 5 (Counter) na Mathematical Set na kalamu
(vii) Raba jozi moja (flat), bukta (kaptula ya michezo) green na T-shirt green kwa ajili ya michezo.(zisizo na maandishi)
(viii) Soksi nyeusi jozi mbili.
(ix) Mto na foronya (blue bahari)
(x) Godoro la Sponji (futi 2½ )
(xi) Shuka mbili (blue bahari) na blanketi moja (au mbili ukijiweza)
(xii) Chandarua (light blue)
(xiii) Ndoo ya Maji,
(xiv) Kijiko, sahani, bakuli na kikombe (½ lita)
(xv) Tai nyeusi mbili (2)
(xvi) Rimu 2 ya karatasi moja yenye mistari na nyingine kwa ajili ya photocopying (A4).
**(xvii) Aje na Sare ya kuvaa baada ya muda wa darasani:-**

Suruali – rangi ya kijivu – 2 (Sample ya kitambaa imeambatanishwa) upana uwe kati ya inch 17 – 18

**N.B. Mwanafunzi asije na nguo yoyote tofauti na sare zilizoagizwa.**

(xviii) Vifaa vya usafi : Soft Broom 1, Reki 1 na Squizer 2. Badala ya jembe na fyekeo alipe sh. 8000 kwenye akaunti ya michango kwa ajili ya kuboresha mazingira na kununulia madawa na ya usafi.

B: Vifaa vinavyopatikana shuleni:

(i) Suruali mbili nyeusi – zitashonewa hapa shuleni kwa TShs. 18,000/= kila moja.

(ii) Sweta maalum (kwa ajili ya hali ya hewa nyakati nyingine kuna baridi sana). Itanunuliwa hapa shuleni kwa TShs. 17,000/= kila moja.

(iii) T-shirt – rangi light blue – 2) sare rasmi ya shule zinapatikana hapa shuleni TShs. 10,000/= kila moja.

(iv) Truck suti light blue 1 yenye nembo na jina la shule. Zinapatikana shuleni kwa Shs. 30,000/=

2. **Simu za mikononi na line haziruhusiwi kabisa hapa shuleni.**

**(i) Kutakuwa na Ukaguzi siku ya kuripoti Shuleni, na ukaguzi wa dharura wakati wowote.**

**(ii) Mzazi atoe Namba yake ya simu kwa mawasiliano ya haraka kupitia Ofisi ya Mkuu wa Shule na katika fomu ya maelezo binafsi iliyoambatishwa.**

**(iii) Mwanafunzi atakayekamatwa na simu, ATAFUKUZWA SHULE.**

3. Mwanafunzi atakabidhi stamp ya kutuma fomu ya maendeleo kwa mzazi wake **(PRF) KILA MUHULA.**

4. Mzazi mwenye E-mail/barua pepe atujulishe.

5. **Cheti cha Daktari:**

Hapa imeambatishwa fomu ambayo **lazima Daktari wa Hospitali ya Serikali** athibitishe na ajaze kuwa huna ugonjwa na kwamba unaweza kumudu masomo yako vizuri. Hivyo hakikisha unapimwa na Daktari wa Hospitali ya Serikali (sio kituo cha afya) kabla ya kufika hapa shuleni na fomu hiyo kuiwakilisha hapa shuleni mara tu unapofika. Hii itakusaidia katika kumlea mwanafunzi kiafya.

6. **Unatakiwa kuja na Fomu ya Uraia au Birth Certificate**

7. **Kukubali Masharti ya Shule:**

Pamoja na barua hii imeambatishwa sheria za shule na fomu ya kukubali sheria hizo, na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Unachotakiwa kufanya ni kusoma sheria hizo kwa makini na kuweka sahihi yako katika fomu ya kukubali kujiunga na shule hii, iwapo unaona umekubaliana na masharti yaliyotajwa.

8. **Shule hii ni ya Serikali hivyo haina dini. Kwa mwanafunzi mwenye msimamo mkali wa kidini, mzazi anashauriwa ampeleke shule za Seminari.**

Mzazi anaruhusiwa kuja shuleni kumsalimu mtoto wake, kila J'Mosi ya mwisho wa mwezi.

9. Wanafunzi wataruhusiwa kwenda mjini Jumamosi ya mwisho wa mwezi.

10.. Mwanafunzi anatakiwa kuhifadhi fedha zake katika Benki yoyote hapa mjini kwa usalama zaidi au Ofisi ya Mhasibu wa Shule.

11. **Karo/Michango ya Ziada:**

(a) Karo ya Shule ni Sh. 70,000/= (Elfu Sabini tu) kwa mwaka. **Zilipwe N.M.B. A/C. NO. 4081200237**

(b) Michango ya ziada:

**N.B.C. A/C. 014103008790**

| | | | |
|---|---|---|---|
| (i) | Tahadhari | TShs. 10,000/= | (hazitarejeshwa) |
| (ii) | Kitambulisho | TShs. 5,000/= | |
| (iii) | Nembo | TShs. 4,000/= | (@ shati 2000/=) |
| (iv) | Uniform | TShs. 103,000/= | (rejea ukurasa wa kwanza) |
| (v ) | Ukarabati wa mezi, viti na vitanda | TShs. 20,000/= | |
| (vi ) | Taaluma | TShs. 20,000/= | - Kila mwaka. |
| (vii) | Matibabu | TShs. 10,000/= | " |
| (viii) | Mlinzi | TShs. 10,000/= | " |
| (ix) | Mahafali | TShs. 10,000/= | |
| (x) | Uzio wa shule | TShs. 50,000/= | |
| (xi) | Jembe na Fyekeo | TShs. 8,000/= | (rejea ukurasa wa 1) |
| (xii) | UMISSETA | TShs. 5,000/= | |
| | **Jumla** | **TShs. 255,000/=** | |

12. **Fedha zote zilipwe kwenye Account zilizotajwa hapo juu. Fedha taslim (Cash) haitapokelewa.**

*NB: Ni sharti ulipe ada na michango ya ziada ndipo uweze kupokelewa shuleni.*

13. Ada, Michango, zilipwe kwenye Akaunti zilizotajwa hapo juu kabla ya tarehe 11.07.**2016** na mwanafunzi aje na stakabadhi ya malipo (Pay in Slip) tarehe ya kufungua shule **tarehe 11.07.2016. Fedha taslim (cash) haitapokelewa.**

14. Mwanafunzi anatakiwa kurudi kwa mzazi au mlezi wakati wa likizo fupi na likizo ndefu. Hivyo mzazi unapaswa kumtumia nauli mwanao mapema kupitia kwenye account ya mwanafunzi/m-pesa 0754090978/Tigo-pesa ya shule tu.

15. Mwisho napenda kukujulisha kuwa unatakiwa kufika hapa shuleni Ilboru Shule ya Sekondari kabla ya tarehe 31.07.2016. kwani zaidi ya hapo hautapokelewa.

**N.B.** (i) Vitu vya gharama kama Kamera, Heater, T.V. na kadhalika haviruhusiwi hapa shuleni.

(ii) Kila mwanafunzi afike tarehe iliyopangwa kufungua shule.

(iii) Mwanafunzi anatakiwa kuja na Stakabadhi za malipo ya ada ya shule, michango yote na vifaa vyote, na kama hatafanya hivyo hatapokelewa.

Ninakutakia safari njema kuja hapa shuleni.

Karibu sana.

**MKUU WA SHULE**

THE HEAD : STER
ILBORU SECONDARY SCHOOL
P. O. Box 5024 ARUSHA

**Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule:**

(a) Wizi

(b) Uasherati na ushoga

(c) Ubakaji

(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vila uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.

(e) Kupigana au kupiga.

(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

(g) Kudharau Bendera ya Taifa

(h) Kuoa

(i) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

(j) Kukataa adhabu kwa makusudi

(k) Kuwa na simu ya mkononi.



THE HEADMASTER
ILBORU SECONDARY SCHOOL
P. O. Box 5024 ARUSHA

**SHERIA ZA SHULE**

Tabia njema ni ya lazima na inatiliwa mkazo hapa shuleni. Mwanafunzi mwenye tabia mbaya hafai kupewa Elimu ya Sekondari au Elimu ya juu. Ni lazima mwanafunzi awe na tabia nzuri wakati wote. Kila mwanafunzi analazimika kutii sheria za shule na kufuata taratibu za shule, pia kuwatii wafanyakazi na walimu na wengine wenye mamlaka. Heshima na adabu kwa mtu yeyote ni kitu cha lazima.

1. Kunywa pombe au kuvuta sigara au kiko ni mwiko.
2. Uzinifu wa aina yoyote ni kosa kubwa sana.
3. Kila mwanafunzi ni lazima awe mtiifu kwa walimu wake wote, wafanyakazi wote, makaka wa shule wote, na wakuu wengine wote. Ujeuri au ubishi wa aina yoyote kwa mwalimu, kaka wa shule au wakuu wengine wote ni mwiko.
4. Hakuna mwanafunzi yeyote anayeruhusiwa kutoka nje ya mipaka ya maeneo ya shule, bila ruhusa (pass) toka kwa mwalimu wa zamu, isipokuwa siku ya kuruhusiwa kwenda mjini rasmi (town leave). Mwalimu au kaka wa shule akimwona mwanafunzi yeyote mjini ana haki ya kumwomba amwonyeshe cheti cha ruhusa (pass).
5. Ruhusa ya kulala nje ya shule, itatolewa na Mkuu wa Shule au Makamu wake tu.
6. Kila mwanafunzi lazima aheshimu kazi za mikono zote ikiwa ni pamoja na bustani, usafi kama vile anavyopaswa kuheshimu masomo ya darasani.
7. Matusi ya aina yoyote, yawe ya kusema au kuandika hayaruhusiwi shuleni.
8. Kila mwanafunzi lazima aheshimu na kutunza mali ya shule, uharibifu wowote utakaotokea utabidi ugharimiwe na mwanafunzi mwenyewe.
9. Sare za shule (uniform) ni lazima zivaliwe wakati wa masomo na wakati wa kuruhusiwa kwenda mjini. Hakuna mwanafunzi yeyote atakayeruhusiwa kutoka nje ya mipaka ya shule bila kuvaa sare za shule, isipokuwa tu kama ruhusa rasmi imetolewa na Mkuu wa Shule.
10. Wizi wowote hauruhusiwi shuleni, iwe ni wa mali ya shule au mali ya mwanafunzi au mfanyakazi.
11. Usafi wa mwili, mavazi, madarasa, mabweni, jumba la chakula (dining hall) jumba la mikutano (assembly hall) jumba la mihadhara (lecture hall) viwanja ni wajibu wa kila mwanafunzi.
12. Ugomvi wa maneno au kupigana ni mwiko shuleni.
13. Kuchelewa kwa aina yoyote bila ruhusa ni kosa, mfano kuchelewa toka mjini, wakati wa roll-call, kuchelewa inspection na kuchelewa toka likizo.
14. Tabia njema shuleni na nje ya shule ni wajibu na ni lazima kwa kila mwanafunzi.
15. Taa za shule na maji ya shule lazima vitumiwe kwa uangalifu.
16. Magazeti au vitabu vyenye picha au maneno yasiyofaa havitakiwi shuleni.
17. Upokeaji au uandishi wa maneno yasiyofaa ni mwiko shuleni.
18. Mwanafunzi yeyote haruhusiwe kuandika barua yoyote kwa Mkuu yeyote mahali popote ya kiofisi bila ya kuipitisha kwa Mkuu wa Shule (k.k. Mkuu wa Shule).
19. Mwanafunzi yeyote haruhusiwe kwenda nyumbani kwa Mwalimu au Mfanyakazi yeyote bila ruhusa ya mwalimu anayehusika.
20. Mwanafunzi yeyote haruhusiwe kutumia vyombo vinavyotumia umeme kama vile redio, heater, pasi, mabwenini au kufanya ufundi wa aina yoyote kwenye umeme bweni au darasani.
21. Ili kuepukana na utoro, kofia **haziruhusiwi** hapa shuleni.
22. Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vya darasani pamoja na 'night preparation'
23. Ni kosa kupiga kelele Smart Area.
24. Ni kosa kugomea mitihani ya ndani na nje.
25. Ni kosa kwa mwanafunzi yeyote kufanya marekebisho ya aina yoyote kwenye sare ya shule.



THE HEADMASTER
ILBORU SECONDARY SCHOOL
P. O. Box 3014 ARUSHA

…………………………………

………………………………

………………………

Tarehe ……………..

Mkuu wa Shule,
Ilboru Sekondari,
S.L.P. 3014,
ARUSHA.

**YAH: KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ILBORU**

Nachukua nafasi hii kulishukuru Taifa letu kwa kunichagua na kunipa nafasi ya kupata Elimu ya Sekonari. Hii ni bahati kubwa na ninaahidi kujifunza kadiri ya uwezo wangu na sitapoteza muda wa masomo darasani au muda wa kazi za mikono kwa kuwa mvivu, au kupuuza shughuli hizo.

Nimesoma sheria za shule na masharti ya kujiunga na shule ya Sekondari Ilboru na ninakuthibitishia kuwa nimeafiki na sheria na masharti hayo na kwamba nitaziheshimu kwa kutokuzivunja kwa makusudi.

Wako mwanafunzi mtiifu,

…………………………………..
Jina na Sahihi ya Mwanafunzi

…………………………………..
Jina na Sahihi ya Mzazi/Mlezi

*NB:* * *Wakilisha fomu hii kwa Mkuu wa Shule mara tu ufikapo shuleni ili iwekwe kwenye jalada lako.*
* Kutakuwepo kikao cha wazazi wote tarehe 08.03.2013.Unakaribishwa kuhudhuria kikao hicho.



THE HEADMASTER
ILBORU SECONDARY SCHOOL
P. O. Box 3014 ARUSHA

*PRESIDENT'S OFFICE*

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

***(To be completed by a medical Officer in respect of all form I and 5 entrants)***

Pupil's full name ……………………………………………………………………………

Age …………………………………………………………………………………………

Blood count (red and white) ………………………………………………………………

Stool examinations …………………………………………………………………………..

Urinalysis ……………………………………………………………………………………

Syphilis test …………………………………………………………………………………

T.B.test ………………………………………………………………………………………

Eye test ………………………………………………………………………………………

Ears ……………………………………………………………………………………..

Chest …………………………………………………………………………………...

Abdomen ……………………………………………………………………………..

Spleen ………………………………………………………………………………………

Additional information: e.g. physical defects, infection, chronic or family diseases etc.

……………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………

I certify that the above is fit to pursue further studies.

Signature ……………………………………..

Designation ……………………………………...

Station ……………………………………

Date: …………………………………….

THE HEADMASTER
ILBORU SECONDARY SCHOOL
P. O. Box 3014 ARUSHA

# MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI.

Ukiwa mwanafunzi na mzazi/mlezi wamekubaliana na masharti yote ya shule, sharti fomu hii isainiwe na watu wanne, ambao ni:

(i) Mwanafunzi mwenyewe: Jina kamili ________________Kidato ___Saini______Tarehe______

(ii) Mzazi/Mlezi: Jina kamili ______________________Saini______________Tarehe_________

(iii) Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa: Jina la Kijiji/Mtaa ________________________________

Jina la Afisa Mtaa/Kijiji: ____________________________________________

Maoni/Mapendekezo kuhusiana na unavyomfahamu mwanafunzi huyu:

--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

Saini ya Afisa Mtendaji ______________________________ Tarehe ______________

Mhuri wa Afisa Mtendaji:

(iv) Mtendaji Kata/Mtaa: Jina la Kata/Mtaa ________________________________

Jina la Afisa Mtendaji Kata/Mtaa _________________________

Saini ya Afisa Mtendaji Kata _________________________ tarehe ___________

Mhuri wa Afisa Mtendaji Kata:



THE HEADMASTER
ILBORU SECONDARY SCHOOL
P. O. Box 3014 ARUSHA

**SHULE YA SEKONDARI ILBORU**

**FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. JINA ………………………………………………........... DINI ………………………………………..........
2. TAREHE YA KUZALIWA……………………........…3. KIJIJI ULIMOZALIWA…………….........
4. TARAFA ULIMOZALIWA ………………… .......5. WILAYA ULIMOZALIWA …………..........
6. MKOA ULIMOZALIWA ………………………........ KAMA UNAKAA MJINI ……………..........
7. TAJA MJI:……………………………..........MTAA………………..BARABARA……………….............
8. JINA LA BABA……………………………….9. KAZI YA BABA…………………......................
10. ANWANI YA BABA……………………………………………………………………......................
11. JINA LA MAMA ……………………………........... 12. KAZI YA MAMA……………………….............
13. ANWANI YA MAMA ……………………………………………………………………....................
14. JINA LA ATAKAYEHUSIKA NA MWANAFUNZI KIPINDI CHOTE CHA MASOMO:

    JINA:............................................................ ANWANI:.......................................................................

    SIMU:......................................................... EMAIL: ..........................................................................

15. SHULE ULIZOSOMA / MADARASA / MADARAKA ULIYOSHIKA

| SHULE ULIZOSOMA | MADARASA | MADARAKA ULIYOSHIKA |
|---|---|---|
| …………………………… | ………………… | ………………………………… |
| …………………………….. | ………………… | ………………………………… |

16. JE, BABA YU HAI? ……………………….............. (NDIYO/HAPANA)
17. JE, MAMA YU HAI? ……………………….............. (NDIYO/HAPANA)
18. JE, UNAKAA NA MLEZI ………………….............. (NDIYO/HAPANA)
19. ANWANI YA MLEZI ……………………………………………………………………
20. KAZI YA MLEZI ………………………………………………………………………
21. ELEZA MATATIZO YA NYUMBANI, YA MAGONJWA, N.K. YANAYOKUKABILI

…………………………………………………………………………………………………………...........

22. UNAFIKIRI MATATIZO HAYO YATATATULIWA VIPI? ……………………………................

    ……………………………………………………………………………………………….................

23. ELEZA MIPANGO YAKO YA MAISHA YA BAADAYE

    …………………………………………………………………………………………………...............

24. MKO WANGAPI KATIKA FAMILIA? (A) WA KIUME ……………………………................

    (B) WA KIKE ……………………….. (C) WEWE NI WA NGAPI ………………….................

    (D) NDUGU WANGAPI WAMEAJIRIWA ? …………………………………………..............

25. KAZI AMBAZO UNGEPENDA KUFANYA BAADA YA KUMALIZA MASOMO

    ………………………………………………………………………………………………….................

26 KAZI AMBAZO USINGEPENDA KUFANYA BAADA YA KUMALIZA MASOMO

    ………………………………………………………………………………………………….................

26. JINA …………………………………… SAHIHI…………….. TAREHE……………..................



THE HEADMASTER
ILBORU SECONDARY SCHOOL
P. O. Box 3014 ARUSHA

## VITABU VYA KUJISOMEA

Mzazi, kama inawezekana, tunaomba umpatie mwanao vitabu vifuatavyo:

MCHEPUO WA HGL (HISTORY, GEOGRAPHY, LANGUAGE)

**(i) HISTORY:**

(a) Longman - History – New version.
(b) Shibital - History One and Two.

(ii) **GEOGRAPHY:** (F) URIO (SUA) – SOIL
(E) JOHN PRITCHARD – PRACTICAL GEOGRAPHY FOR AFRICA
(a) WAUGH,D – GEOGRAPHY, AN INTEGRATED APPROACH
(b) MORGAN - HUMAN ECONOMIC GEOGRAPHY
(c) BUNETT, R – PHYSICAL GEOGRAPHY
(d) MONKHOUSE – PRINCIPLES OF PHYSICAL GEOGRAPHY.

**(iii) LANGUAGE:**

(a) Advanced Dictionary of Contemporary English
(b) A practical approach $2^{nd}$ edition – Nicholaus Ashel.
(c) Advanced Level English – Oxford.
(d) Writing Skills – Kiura.

## VITABU VYA KUJISOMEA

**MCHEPUO WA PCB, PCM (PHYSICS, CHEMISTRY and BIOLOGY or PHYSICS.**

**PHYSICS:**

(a) Cand, S (2008) Principles Of Physics For Class x11 & x12, New Delhi.
(b) Nelkon & Parker (1995) Advanced Level Physics $7^{th}$ Edition. Longman International Education.
(c) Duncan, T, New Understanding Physics for A-Level.

**CHEMISTRY:**

(a) Conceptual Chemistry – Chand S.K.
(b) Chemistry in Action – Michael Freematle
(c) Physical chemistry for A-Level and Undergraduate: Mkayuba and Ddungu.
(d) Advanced Inorganic Chemistry Part I and II – TIE.
(e) Soil and Environmental Chemistry.

**BIOLOGY:**

(a) Yaylor, D. J. (1997) Biological Science, Cambridge University Press.
(b) Susan Toole – Understanding Biology.
(c) Msaki, L (2003) Cell Structure.
(d) Msaki, L (2003) Systematics and Classification.

**MATHEMATICS:**

(a) Backhouse, Pure Mathematics 1
(b) Backhouse, Pure Mathematics 2
(c) Shayo Leonard, Advanced Mathematics Vol. I.
(d) Chand, S, Mathematics for Class xii.
(e) Understanding Mathematics.



THE HEADMASTER
ILBORU SECONDARY SCHOOL
P. O. Box 9014 ARUSHA